


KASI UKUAJI HUDUMA ZA FEDHA MTANDAO INAVYOAKISI DIRA 2050

Na Mwandishi Wetu

USAMBAAJI wa huduma za intaneti umewezesha ukuaji wa uchumi kidijitali kwa kuongezeka kwa huduma za pesa mtandao kwa asilimia 5.3 kwa kipindi cha robo mwaka inayoishia Septemba 2025, ambazo zimetoa ajira na kuwezesha upatikanaji wa huduma za fedha.

Kasi ya ukuaji wa huduma za pesa mtandao unakwenda sambamba na DIRA 2050 ambayo imelenga kuwa na nguvukazi yenye ubora ambayo itatumia fursa za kiuchumi kidijitali kwa kushirikiana na sekta binafsi. Ripoti ya Takwimu ya Hali ya Mawasiliano iliyotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kufikia Septemba 2025, inaonesha idadi ya akaunti za pesa mtandao ambazo zilitumika angalau mara moja kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita iliongezeka kwa asilimia 5.3 kutoka akaunti milioni 68.1 katika robo mwaka iliyoishia Juni 2025 hadi milioini 71.7 Septemba 2025.

Aidha, akaunti za pesa mtandao zimeongeka kwa watoa huduma wote kwa kipindi cha miezi mitatu ambao ni M-Pesa, Mixx by Yas, Airtel Money, T-Pesa , HaloPesa na Azam Pesa. Wakati akaunti za pesa mtandao zikiongezeka kwa wastani wa asilimia 1.6 kwa mwezi katika robo inayoishia Septemba




2025, idadi ya miamala imeendelea kuongeza kwa kila mtandao.

Aidha, idadi ya usajili wa pesa mtandao kwa robo mwaka iliyoishia Disemba 2024 ilikuwa 63,207,569 huku idadi ya miamala ikiwa ni 1,100,700,205.

Pia Machi 2025 idadi ya akaunti zilikuwa 66,542,276 na idadi ya miamala ni 1,366,334,366, huku Juni ikiwa ni akaunti 68,059,290 na miamala 1,392,683,175, huku kwa Septemba 2025 ikiwa ni akaunti 71,662,333 na miamala 1,694,032,906.

Kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2020 - 2024 usajili wa miamala ya pesa mtandao iliongezeka, jambo linaloonesha ukuaji wa uchumi wa kidijitali wenye manufaa kwa mwananchi mmoja mmoja. Takwimu zilizopo kwenye ripoti hiyo ya TCRA zinaonesha kuwa mwaka 2020 kulikuwa na akaunti 32,268,630, huku miamala ikiwa ni



3,412,210,062. Aidha, mwaka 2021 akaunti zilikuwa 35,285,767 huku miamala ikiwa ni 3,752,084,894, mwaka 2022 akaunti zilikuwa 40,953,496 na miamala 4,195,899,414. Mwaka 2023 akaunti zilikuwa 52,875,129 huku miamala ilikuwa 5,273,086,154, na mwaka 2024 akaunti zilikuwa 63,207,569 na miamala 3,737,202,434.

Mabadiliko haya yanajitokeza wakati ambao idadi ya laini za simu za mkononi na za mezani ambazo zilitumika kwenye huduma ya mawasiliano angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita zimeongezeka kutoka milioni 92.7 Juni 2025 hadi milioni 99.3 Septemba 2025.

ISEMAVYO DIRA2050

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 yenye vipengele vinane, ikiwemo kipengele cha vichocheo vya kufikia malengo ya DIRA kipaumbele kikiwa mageuzi ya digitali na kuanishwa kwenye Ripoti ya Takwimu ya Sekta ya Mawasiliano katika mabadiliko ya kiuchumi yanayosukumwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tangu aingie madarakani Machi 2021.

Aidha, inaeleza kuna fursa kubwa ya kuharakisha katika karne ya 21 kuelekea maendeleo ya teknolojia za kidijitali, ili kufikia malengo ya Dira 2050 kwa kuboresha ukuaji wa maendeleo kupitia uchumi na kuimarisha huduma za kijamili kwa kutumia teknolojia kwa ufanisi.

Pia DIRA 2050 inaelenga kuwa Tanzania itaongeza ushindani wake, itapanua wigo wa uchumi



Dkt. Jabiri K. Bakari | Mkurugenzi Mkuu - TCRA

na huduma, kuboresha uwezo wa kufanya maamuzi, kuongeza huduma jumuishi za kifedha, kuendeleza matumizi ya huduma za kidijitali katika sekta mbalimbali na kujenga uwezo wa kutumia teknolojia mpya zinazoibuka.

“Tanzania imepiga hatua kubwa katika maendeleo ya teknolojia kidijitali, ikidhihirishwa na kuongezeka kwa matumizi ya huduma za kifedha kupitia simu za mkononi, upatikanaji wa intaneti yenye kasi na maendeleo ya serikali mtandao ambayo kwa kiasi kikubwa yameboresha utoaji wa huduma kwa umma.



“Huduma za kifedha kupitia simu za mkononi zimeleta mapinduzi kwenye sekta ya fedha za mkononi, jambo ambalo imesaidia watu wengi hasa waishio vijijini.

Aidha, teknolojia za kidijitali zimeleta mabadiliko katika utoaji wa huduma za afya, elimu na kilimo na hivyo kuongeza ufanisi katika utendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi.

WANUFAIKA

James Mangachi anaemiliki duka la huduma za kifedha eneo la Sakina Mkoani Arusha anasema: “Kwasasa ninailiki ofisi yangu ya huduma za kifedha ambapo nimeajiri watu wanne ambao wangukuwa mtaani kwa kukosa kazi. Mimi ninapata kipato cha kuendesha maisha yangu, nalipa kodi na nimejairi watanzania

wenzangu.”

Ramadhani Mwinyimvua wakala wa huduma za kifedha eneo la Kiluvya wilayani Kisarawe mkoani Pwani, anasema “Kazi hii imenipa ajira, naendesha familia na kusomesha watoto kwa kufanya huduma za kifedha, serikali imefanya jambo zuri kuimarisha huduma za kifedha nasi tunaona faida ya uchumi wa kidijitali.”

WASOMI

Profesa Mshiriki kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. George Kahangwa anasema mabadiliko ya kiuchumi ni makubwa kwa kuwa imeokoa muda ambao ni pesa, kwa kuwa zamani ilikuwa ni lazima kwenda kuonana na karani au muhudumu wa benki ndipo upate fedha lakini teknolojia imesaidia watu wanajihudumia kwa simu, wameweka akiba, wamewekeza na kununua hisa kwenye kampuni na taasisi mbalimbali.

“Teknolojia imeleta mapinduzi makubwa katika utoaji na ufikiaji huduma za kifedha, unaweza kupata huduma nyingi sana, tunapata faida ya kurahisisha kazi, kuna muda mwingi ulipotea kwa kwenda kuwafuata wahudumu, unakaa kwenye foleni na sasa unapata huduma kwa urahisi,” anasema.

Aidha, Prof. Kahangwa anasema uchumi wa dijitali umeleta watoa huduma wa fedha wengi ambao



wasingeajiriwa kwenye taasisi za fedha lakini wamejiajiri kwa mitaji midogo wanatoa huduma za kifedha ambazo huenda wasingepata ajira kokote, na wanaendesha maisha yao, na wamefikisha huduma kwa wananchi.

TCRA imechukua jukumu la kuwaandaa watoto kutokea katika shule za awali hadi vyuo vikuu kupitia klabu za kidijitali ili kushiriki vyema katika kubuni suluhisho za teknolojia mbalimbali. Matajiri wakubwa duniani wamenufaika kwa kuwa wazalishaji wa teknolojia.

Naye, Mhadhiri katika Taasisi za Stadi za Maendeleo katika Chuo Kikuu

cha Dodoma (UDOM), Dk. Leonce Mujwahuzi anasema uchumi wa kidijitali umeleta mageuzi makubwa kwenye maisha ya watu kwa kuokoa muda ambao mtu angutumia kwenda kufuata huduma za kifedha.

“Kabla ya kuboreshwa kwa huduma za pesa mtandao ilikuwa lazima mtu asafiri au kutembea kwenda benki au taasisi ya fedha, ajaze makaratasi, lakini kwasasa anaweza kulipia huduma kokote aliko kwasababu ya maboresha ya huduma za kifedha,” amesema.

Mujwahuzi ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi UDOM Saccos Limited, alisema kwasasa biashara inafanyika kwa kutumia mtandao, na unapokwenda kwenye duka lolote kuna Lipa Namba, na mtu anafanya bishara kokote alipo, anatangaza bidhaa, anauza na kupata fedha zake kirahisi kwasababu huduma za kidijitali zimeimarika.



Skani kupakua
Ripoti ya Takwimu
ya Sekta ya
Mawasiliano